

**HOTUBA YA JAJI MKUU WA ZANZIBAR  
MHE. OMAR O. MAKUNGU  
ILİYOTOLEWA KATIKA UFUNGUZI WA MKUTANO MKUU  
WA ZAJOA 2014 ILİYOTOLEWA KATIKA HOTELI YA  
UTALII, MARUHUBI, TAREHE 1 MACHI, 2014**

**MHESHIMIWA MWENYEKITI  
WAHESHIMIWA WAJUMBE.**

**ASSALAMU ALAYKUM:**

Kwanza, kabisa ningependa kuanza hotuba yangu hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema, salama, amani na utulivu katika nchi yetu na leo tumeweza kukutana hapa kufanya shughuli zetu tulizozipanga.

Pili, Ninashukuru sana kupewa nafasi hii adhimu ya kuwa Mgeni rasmi katika ufunguzi wa Mkutano huu wa mwaka wa ZAJOA. Ninasema ni nafasi adhimu kwa sababu Viongozi tupo

wengi lakini bado nimepewa mimi kwa mara nyengine heshima hii.

Ahsanteni sana.

### ***Ndugu Mwenyekiti.***

Napenda niwashukuru kwa dhati kabisa Majaji, Mahakimu na Makadhi wote kwa kushiriki kikamilifu na kufanikisha mkutano wa EAMJA uliofanyika August, mwaka jana. Pia kwa kufanikisha "***Law day***" ya mwaka huu. EAMJA Ulikuwa ni mkutano wetu wa kwanza kuandaa lakini umekuwa na mafanikio kiasi ambacho kila mtu anataka afanye mkutano Zanzibar. Kwa taarifa tu wiki chache zilizopita tumeandaa mafunzo (***training***) ya Majaji na Mahakimu wa Afrika Mashariki, Mafunzo ambayo yalitakiwa kuandaliwa na wenzetu wa Tanzania Bara. Aidha ICJ Kenya

wameomba mkutano kuhusiana na mambo ya utekaji meli (***pirates***) ifanyike Zanzibar, mwaka huu.

Naomba tuendeleo kushirikiana kwenye mambo haya ili tuweze kuiletea sifa Zanzibar kama nchi na Mahkama ya Zanzibar kama taasisi.

Kuhusu "***Lawday***" ya mwaka huu sote ni mashahidi kuwa hotuba nyingi zilizotolewa ziliilenga Mahkama. Hii ni kutokana na udhaifu wa utendaji wa baadhi yetu. Ni vyema tukajirekebisha vyenginevyo kila siku tutakuwa ni wa hanga wa "***Law day***" tulizozianzisha wenyewe.

### ***Ndugu Mwenyekiti.***

Najua kuwa Mkutano huu ni Mkutano Mkuu wa mwaka wa ZAJOA hatuna budi kujadili mambo yetu kwa uwazi na kwa

umakini zaidi. Pia tuweze kuchambua ripoti zitakazowasilishwa mbele yetu na Katibu na Mshika Fedha. Ripoti hizi ndizo zenye kutoa tathmini ya mambo tuliyoyafanya kwa mwaka huu.

### ***Ndugu Mwenyekiti.***

Napenda kueleza kuwa tumepata wanachama wapya katika Jumuiya yetu. Hawa si wengine ila ni Mahakimu na Makadhi wapya walioajiriwa miezi kadhaa iliyopita. Naomba niwakaribishe katika ZAJOA na wajisikie kuwa wapo nyumbani. Nawaomba washirikiane nasi katika kukiendeleza chombo hichi.

### ***Ndugu Mwenyekiti.***

Nafahamu kuwa mwisho wa siku tuna agenda ya uchaguzi wa viongozi wa taasisi yetu hii. Hii ni agenda muhimu na inabidi tuipe umuhimu wake. Nawapongeza wale wote ambao

wameamua kuchukua fomu ya kugombea nafasi mbali mbali. Najua kampeni za chini chini zimeanza. Naomba nitoe indhari hapa kuwa tuwe makini katika kuchagua viongozi wanaofaa kiuwezo na kimaadili.

Uchaguzi uliopita uligubikwa na majungu na fitna zilizopandikizwa na baadhi ya Mahakimu wa Mahkama ya mwanzo, jambo lilipelekea kupata baadhi ya viongozi wasio na uwezo na hivyo kuporomosha uwezo na hadhi ya ZAJOA kikanda. Naomba sana mara hii fitna na majungu tuyawache kwani hayasaidii katika kuimarisha taasisi yetu. Najua bado kikundi hichi cha Mahakimu wa chache wa Mahkama ya mwanzo kipo na kinaendeleza fitna na majungu kwa kushirikiana na baadhi ya Majaji na Mahakimu wa ngazi nyengine ili kuuu taasisi hii pamoja na kuiletea aibu Mahkama. Napenda niwaeleze kuwa mimi nawajua na kama Mkuu wa muhimili huu wa Mahkama nitakuwa tayari kupambana nao kwa hali zote. Mimi sitakubali kuona

taasisi hii ya ZAJOA inakuwa **'influenced'** na hawa watu wachache. Nawaomba Majaji, Mahakimu na Makadhi tuwe macho na wenzetu hawa ambao hawatutakii mema na wanadhamira mbaya ya kutuvuruga. Nawaasa pia Mahakimu wavya kutojiingiza katika mtego huu.

### ***Ndugu Mwenyekiti.***

Ningependa kutumia nafasi hii kwa heshima na busara kuisitiza umuhimu wa kuchagua viongozi watakaoweza kuiongoza Jumuiya yetu vizuri kitaifa na kimataifa. Na tukitilia manani kuwa Jumuiya kama hizi zipo Kenya, Uganda, Tanzania Bara, Burundi na Rwanda na tunatakiwa kufanya kazi pamoja katika makongamano, mikutano n.k.

### ***Ndugu Mwenyekiti.***

Nisingependa kutumia muda zaidi wa kutoa hotuba. Nafikiri haya niliyoyasema yanatosheleza na naamini yatasaidia kwa njia moja au nyengine kuimarisha ZAJOA.

Naomba nimalizie kwa kuwaomba wote tufuate maadili ya kazi na tuache kujiingiza katika mambo ya rushwa, utovu wa nidhamu, ubinafsi na mengineyo.

Baada ya kusema hayo machache, napenda kuchukua nafasi hii kutamka kuwa Mkutano Mkuu wa mwaka wa ZAJOA umefunguliwa.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.